
Barazani. Kitabu cha 25.



# HABARI za WAZARAMO

S 17
12187

Kiasi chake Senti 20.

# Vitabu vya barazani.

No. 1. **David Livingstone.** Maisha ya msafiri aliyeanza kutangaza maneno yake Bwana Yesu upande wa ziwa la Nyasa na la Tanganyika. Sh. 0,20

No. 2. **Ufalme wa Mbingu umekaribia.** Kitabu kilicho na picha 12 za habari za Agano Jipya. Sh. 0,50

No. 3. **D. Martin Luther.** Maisha yake yule shujaa hodari wa Yesu Kristo aliyetuonyesha maana yake kumtegemea Yesu vema. Sh. 0,50

No. 4. **Bwana von Bodelschwingh.** Mtu aliyezidi kusaidia wagonjwa kwa ajili ya Yesu. Sh. 0,20

No. 5. **Muhamadi au Kristo?** Maneno mafupi ya kweli ya Muhamadi. Sh. 0,20

No. 6. **Ludwig Krapf.** Misionari aliyefika 1848 Mombasa, akianza kutangaza utume mwema wa Kristo upande wa East Afrika. Sh. 0,20

No. 7. **Habari za Wakristo wa zamani walioteswa kwa ajili ya imani.** Wale watu waliumizwa, wakauawa, lakini walikufa na furaha na mfalme wao Yesu. Sh. 0,20

No. 8. **Konstantino na Yuliano wafalme wa Kiroma wa kale.** Wakubwa wa nchi walitaka kuzuia ufalme wa Mungu, anayeeneza ni Mungu pekee. Sh. 0,20

No. 9. **Aurelyo Augustino.** Mkristo wa nchi ya Afrika, ameshindwa akawa mtumishi wake. Sh. 0,20

No. 10. **Sadhu Sundar Singh.** Mhindi alikuwa mwonaji wake mkuu Bwana Yesu. Sh. 0,50

No. 11. **Ana na Dora, wanawake wawili wa Kikristo,** wanasaidia waume katika kazi zote. Sh. 0,20

Po 05-25

Barazani — Kitabu cha 25.


# Habari za Wazaramo.



Kimetolewa na misioni ya kievangelishe.

Kinapatikana
kwa Usambara-Agentur, misioni ya Lwandai
P. O. Lushoto, T. T.

1935.




48/570
Stadt- u. Univ.-Bibl.
Frankfurt/Main

# Habari za Wazaramo.

Zimeandikiwa wenzetu Wakristo wa Kizaramo na wenzao.

Uzaramo nakupenda, Uzaramo nakupenda sana, ndivyo walivyoimba Wazaramo wa Maneromango, kwani wanapenda „ukaye“ wao. Kila mtu hupenda nchi yake, alikozaliwa na kukua. Akiwako nchi nyingine, husema: Sasa nakwenda kwetu. Basi mtauliza: Uzaramo uko wapi? Ukijua kusoma ramani, utazame nchi ya Tanganyika Territory, utauona mji mkuu Daresalama pwani, utauona kusini mto Rufiji na kaskazini mto Ruvu, basi kati ya mito hiihii kandokando ya pwani ni nchi ya Wazaramo, ndio Uzaramo. Lakini watu wa pwani, kama wa Daresalama au wa Ukindu au wa Bagamoyo, ukiwauliza: Enyi wenzangu kabila yenu ni kabila gani? Watajibu: Sisi Waswaheli, Uzaramo uko huko mbali bara. Wanaona soni kutajwa Wazaramo, kwani husema: Wazaramo na washenzi ni wamoja. Kweli kuna Wandengereko kule Rufiji, kuna Wamashomvi Daresalama, kuna Wanyamwezi, ndio watani wa Wazaramo, au „wagongo“ wao. Pana makabila mengi, lakini walio wengi Uzaramo ni Wazaramo. Nao wasione soni kuitwa Wazaramo, ila wapende kabila lao, walimozaliwa. Si vibaya kuwa Mzaramo, ila vibaya ni kuficha kabila lako. Sababu hii enyi wenzangu Wazaramo, msiisahau asili yenu na msiwabeze Wazaramo wenzenu, „ukaye wenu“ ni Uzaramo, basi. Sasa nitawakumbusha mimi, niliye mgeni, habari zenu kama niwezavyo.

Imepita labda miaka 200, zamani zile hawajakuwapo Wazaramo katika Uzaramo. Kweli mimi

na nyinyi tulikuwa hatujazaliwa enzi ile, lakini „wahenga“ wenu wametusimulia habari za kale, hata wao wameambiwa na wazee wao. Wangalijua kuandika, wangetuandikia habari zingine zingine, lakini hivi tumepata habari kwa midomo tu. Leo haja ya kila mtu ni kufika Daresalama na kuona mambo ya leo kule, nyumba kubwa za Wazungu na meli za Ulaya na mambo mengine ya vioja. Mtu akitembea mjini, huona gari la moshi hata ndege ya Ulaya, hufika sokoni, atazame kila namna ya chakula, hamu itampata, anunue chakula kitamu. Ataona maduka ya Wahindi mengi sana, na vitu vilivyowekwa mle, hatanunua kitu cha mambo ya leo, ijapompasa kukopa? Kweli enzi ya leo imegeuka kabisa. Zamani zile Daresalama haukujulikana, kwani mahali pake palikuwapo kijiji kidogo tu, wavuvi wachache na Waarabu wachache na Wahindi nusu tu, basi. Kile kijiji kiliitwa Mzizima. Zamani zile Bagamoyo ulikuwa mji kweli wenyi biashara nyingi. Kutoka Unguja bizaa zote zikafika Bagamoyo kwa madau ya Waarabu na Wahindi, nao wenyeji wa nchi ya pwani walikuwa Wamashomvi, makabila mengine walikuwa Wambwela na Wamwambau, waliokaa vilevile pwani. Lakini msizani, kama nchi ilitengemana, machafuko mengi yaliingia katika nchi sababu ya kuchuuza watumwa. Utumwa umewasumbua watu wengi na kuharibu nchi na mali. Waarabu na Wahindi wakafanya misafara yao kutoka Bagamoyo, wakapeleka bizaa zao bara, wapagazi wengi, mia na mia wakatuta mizigo yao, askari na bunduki wakawasindikiza. Hivi Waarabu wakafika mpaka Tabora, ulioitwa Kazee zamani zile. Wakafika mpaka ziwa la Tanganyika na Ujiji, hata nchi ya Kongo ng'ambo ya ziwa, wanakokaa Wamanyema. Kurudi wakarudi na watumwa, wakawauza Unguja na pengine. Wakubwa wa nchi, masultani na „wandewa“, nao wakaingia katika biashara hii



wakifanya urafiki na Waarabu. Waliotaka labda chumvi, wakauza ndugu, wapate chumvi, au wakauza pembe na ngozi, wapate ushanga au nguo au chumvi. Hivi Waarabu na Wahindi wakapata kuwa wenyeji wa bara, kwani walikuwa wamefika zamani sana pwani, maboma yao yalikuwa Mombasa na Lamu na Kilwa na pengine. Kutoka kule wakaingia nchi ya bara. Nazani, mmejua hata kabila la Wareno, nao wamefika zamani chi yetu, wakajenga maboma yao pwani, Kilwa-Kisiwani na Mombasa, wakashindana na Waarabu miaka kama mia mbili, (tangu 1500 mpaka 1700). Leo wanakaa katika nchi ya Mozambigi (Portuguese East Africa), iliyo kusini ya Tanganyika Territory, petu walishindwa na Waarabu walihama.

Zamani zile makabila ya Waafrika hayakukaa nchi zao za leo, yalikuwako machafuko mengi ya kuhamahama, kwani watu wa kusini, waitwao Wazulu, wakatoka kusini na kuwashambulia wenyeji wa kwetu Tanganyika, wakawanyang'anya ng'ombe na mali, nao wenyeji wakakimbia na kutafuta nchi nyingine, wakae. Mmewafahamu Wangoni na Wamafite kuwa wao ni mbegu ya Wazulu. Je mnaonaje, nchi ilitulia zamani? Ilikuwa vita popote, ndiyo nchi ilikuwa imejaa shida tupu.

Basi tangu mwaka wa 1850 Wazungu waliingia nchi yetu, wakaigundua nchi. Walifika Unguja kwanza, halafu wakavuka wakafika Bagamoyo kwa madau yaleyale ya Waarabu. Huko Bagamoyo wakaitengeneza misafara yao, wakaandika wapagazi wakasafiri bara, waione nchi na mito yake na makabila yake na milima yake na kila jambo. Tangu enzi ile nchi ikageuka. Hapo kukaanza kutulia kidogo, kwani vita zikaanza kwisha. Lakini Mzizima ulipataje kuwa Daresalama? Kule Unguja Waarabu wa Maskati walitawala, masultani wao waliitwa „Sayidi“. Kwa sababu hii hata leo watu huamkiana hivi: Mwi-

nyi. Anajibiwa: Mwinyi mkuu Sayidi. Ndivyo wanavyoheshimiana. Basi sultani Sayidi Bargashi akafika Mzizima, akaiona kuwa ni bandari nzuri, akajenga nyumba yake kubwa, apate kupumzikia na kupunga hewa. Nyumba hii iko Daresalama mpaka leo. Akauita mji huu: Daresalama, maana yake bandari ya salamu. Tangu siku zile mji huitwa Daresalama. Hatujui tena Mzizima, ila Daresalama tu. Masultani wengi walikuwa wamewekwa na wale Sayidi wa Unguja, wakaitwa majumbe, nao masultani wa Pazi wakaitwa „wandewa". Lakini habari hizo zitaandikwa baadaye.

## Mwanzo wa Wazaramo.

Je, vipi walivyoingia Wazaramo katika nchi hii ya karibu yake Daresalama? Hata Wamashomvi walikuwa wafanya biashara tangu zamani. Waliwatuma wapagazi wao hata bara. Kutoka Mzizima misafara yao ikapita nchi hii, inayoitwa leo Uzaramo. Lakini kabila la Wakamba ndio waliokuwamo katika nchi, nao walikuwa wakali wakafanya fitina siku zote, askari wao wakawanyang'anya wapagazi wa Wamashomvi mizigo yao na kuwapiga, ikawa hivyo hivyo siku zote. Wamashomvi walipata hasara kubwa sana, tangu hapo walikasirika. Nao hawakuwa wapiganaji, ila waoga, wala hawakuwa na askari wa kuwasaidia, wawafukuze Wakamba. Kwa sababu hiyo wakatafuta askari hodari, wawashambulie Wakamba. Lakini kila walilofanya lilikuwa la bure, Mkamba hakushindwa, na matata ya nchi hayakwisha. Wamashomvi wakasikia, kama yuko mpiganaji hodari, sultani Pazi Kilama, aliyekaa Lukelele nchi ya Kutu ng'ambo ya Ruvu. Yeye alikuwa kweli mpiganaji, mtu hodari. Pazi alikuwa mwinda tembo na chui na simba, hakuwa na woga wowote, kwa upinde wake na mishale na mikuki na shoka alikwenda kuwinda nyama. Alikuwa na



mbwa mkubwa kama chui, popote alipokwenda bwana wake, akamfuata, hapakuwa na mbwa kama yeye. Pazi alikuwa akibeza mlufia, hakuvaa kofia, ila nywele zake zilikuwa kama kofia yake, kwani hakuzinyoa au kuzikata, hakutumia wembe siku zote. Nazani, watu waliomwona Pazi, walishikwa na woga sana wakifikiri: Lo, huyu ni shetani. Pazi alikuwa na maumbu wawili: Mlalukali na Nyapazi. Lakini sijui sawasawa kama umbu ni mmoja mwenyi majina mawili au ni kweli umbu ni wawili. Nao walikuwa hodari kama ndugu yao, walikwenda na kumsindikiza Pazi safari ya kuwinda nyama au safari ya vita. Sababu ya ushujaa wao, majina yao yamevuma mpaka leo, mtawala wa kike wa enzi ya leo ni Mlalukali na Nyapazi. Basi sifa ya yule Pazi ikafika hata Daresalama, nao Wamashomvi wakaona: Inafaa tumwite yeye, awafukuze Wakamba. Wakawatuma watu wao kwa Pazi, wamwombe, aje awasaidie katika shida zao. Wakachukua bizaa na chumvi na vitu vingine, wampelekee zawadi. Pazi akawapokea vizuri, nao wakamwamkia kama desturi: Simba mwenee? Naye akaitikia: Ulembo umala mwaka. Maana asijivune, anaitikia: Ulembo wake umekwisha zamani. Basi wakasema shauri lao, lakini Pazi mjanja akauliza: Je, nitapata nini nikiwasaidia? Wakamtolea zawadi zao na kusema: Nchi ya pwani ni nzuri sana? chakula kingi, utafurahi, ukifika pwani. Akakataa; inasemwa, ya kama wakampa chumvi, alambe. Pazi alikuwa hajaijua chumvi, akailamba, akaona utamu wake, wakalamba nao wenziwe na maumbu yake, wote wakastaajabu na kuingiwa na hamu ya kwenda pwani sababu ya chumvi. Hivi Pazi akakubali kwenda pwani, awashambulie Wakamba.

Basi Pazi na Nyapazi na mbwa na askari wake wakasafiri kwenda vitani, wakapita nchi ya Kisanga na Kinyanguru. Pale Pazi akasema maneno mnayo-

yajua nyinyi nyote hata leo: Kibwe banduka, ulanga wela! Mara jiwe likapasuka na mbingu zikafunuka. Mpaka leo unaweza kuona nyayo zake Pazi na za mbwa wake katika jiwe lile. Mimi sikuona, ila nimeambiwa tu. Pazi alijua tu ya kama atamshinda Mkamba, lakini hakumshinda safari ile ya kwanza, ilimpasa kurudi nyumbani pasipo kitu au mateka. Akawatafuta wasaidia, akawaendea Wadoe, waliopakana naye. Katika nchi yao alikuwako jumbe mmoja, jina lake Mwene mhila, yeye akatafuta mke akamposa Mlalukali, umbu lake Pazi, naye Pazi akakubali, kwani alifikiri hivi: Nikimpata Mwene mhila, kuwa shemeji, atanisaidia kuwapiga Wakamba pwani. Mwene mhila akamwoa Mlalukali, akakubali hata kwenda vitani pamoja na Pazi. Wadoe walikuwa wakila watu, walizoea sana nyama ya watu, walifanya hivi: Wakafunga kamba kutoka mjini pao mpaka njiani, wakaipitisha ile kamba njiani, chini kwa chini, penyi mji wakaifunga kamba penyi kengele ya ng'ombe. Wasafiri waliopita njiani hawakuona ile kamba, wakaigusa tu, mara kengele kule mjini ikalia. Hivi Wadoe wakajua, wako watu njiani, wakaendea upesi wasafiri na kuwakamata na kuwachinja na kuwala. Ndivyo nilivyosikia na kuambiwa na Mdoe mwenyewe. Wadoe wakali wakaenda vitani pamoja na Pazi na watu wake. Wakapita mji Kaole na kuzunguka katika nchi yote ya Wazaramo. Wadoe kazi yao ni kujificha na kuwavizia watu na kuwakamata, wakawachinja kama mbuzi. Nchi ikajaa hofu, watu wakakimbia na kusumbuka sana, wote wakalia: Oyo Mdoe, Mdoe kokwidza. Mpaka leo watu hawajasahau mambo hayo. Pazi na askari wake walikuwa wakipigana waziwazi na Mkamba na kumshinda, wazee wanakumbuka hata ile miji palipokuwa vita zamani iliyo kali, kama Sungwi na Mkamba na pengine. Mji wa Mkamba uko mpaka leo pale palipokuwa na kambi ya Wakamba na boma lao, lakini Pazi akapasua boma lao akafukuza adui, nao Wakamba wakakimbia, wasionekane tena katika nchi yetu. Wakamba wanakaa sasa katika nchi ya Kenya.



Basi Pazi akawatuma watu wake kwa Wamashomvi, wampe mshahara wake. Nao wakamwuliza: Unataka kiasi gani? Akasema: Nataka bizaa, kanga na nguo nyingine, zijae toka chini penye shina mpaka juu penye ncha ya mvinja. Wakakubali, siku moja wakakusanyika wakajaza nguo kila namna kutoka chini mpaka juu, lakini nguo hazikufika ncha ya mvinja. Wakasema: Kwanza tutume dau letu, liende Barawa, lilete zaidi. Lakini Mlalukali akasema: Sivyo hivi, ila sisi na watoto wetu tupate kila mwaka fungu letu, hongo la Pazi. Mmashomvi akakubali shauri hilo. Pazi akarudi nchini kwake, watu wake wakakaa Uzaramo, lakini kila mwaka wakaenda Daresalama kupokea hongo la Pazi. Alipokufa yeye, wakaenda majumbe wake, wapate lile hongo. Watu husema, kama mwisho hongo lilikuwa reale moja tu, mimi sijui. Ndugu na jamaa zake Pazi walikuwa wamewekwa „wandewa" katika nchi, lakini wale majumbe ni wakubwa, waliowekwa na Sayidi. Hata leo wako wandewa, wanaitwa Pazi. Basi watu wa Pazi wakasema: Sisi tumezaana katika nchi hii, sisi ni Wazaramo, na nchi yetu ni Uzaramo. Lakini wamezoea hata kujitaja Wapazi, kwa kizaramo ni Wamhadzi. Nao walio na mwiko wake Pazi ni kweli wa „mtala" wake, mtala hufuata baba, ukoo hufuata mama. Na mwiko wa Pazi Kilama ulikuwa „mpelembo". Kusudi natia hata maneno ya kizaramo, kwa maana Wazaramo wakumbuke zaidi habari zao.

Sasa tukumbuke habari za koo za Wazaramo, kwani Wazaramo si ukoo mmoja tu, ila koo nyingi. Ukoo wa Walugoma unakaa zaidi kule Kisangile kwa Kibasila. Nimeambiwa, kama Lugoma alikuwa mchonga ngoma na mpiga ngoma wakati wa Pazi Kilama.

Basi watoto wake ni Walugoma. Wako Wabena walioko Maneromango, wale, nimeambiwa, walikuwa hodari, kwani vitani walikuwa wabena migoha, maana yake: Wamevunja mikuki kwa nguvu zao. Sijui, kama wamefika kwa nguvu, ila naona, ni watu waliotoka bara, nchi ya Ubena. Wamindu nao wametoka katika milima ya Mindu kule Morogoro, kwani mlima wa Mindu ulikuwa na majoka makubwa mengi, waliyowauma watu, kwa hiyo watu wakahama. Wamhangala ndio wale, waliotumia dawa ya mti wa mhangala, unaoota penye matawi ya miti mingine, unaiua ile miti. Basi dawa ya mhangala, wanasema, inawalinda watu, wasife vitani, wajapochomwa na mikuki au mishale. Wavilindi, ndio waliotoka pwani penye Kilindini. Wampalanguru, ndio waliopata vichwa vya nguru tu, mateka ya vita yalipogawanywa. Wavilima wanasema: Sisi tumetoka kweli vilimani Kutu, sisi ni Wapazi kweli. Wahemezi ni watu, wanaohemea, kuhemela, maana yake kutafuta kazi na chakula huko na huko katika nchi, ndio watembezi sababu ya chakula. Walukali ni watoto wa yule Mlalukali. Yatosha hayo, pana koo nyingi nyingine bado, lakini mnazijua wenyewe. Basi sasa tutazame desturi na sheria za Wazaramo: Ukoo au lukolo la mama ni ukoo wa watoto wake, wanasema: Tunafuata bibi, lakini ukoo wa bibi ni ukoo wa mama vilevile. Lakini ukoo wa baba ni mtala wa watoto, watu wengi, hata Wazaramo huchanganya ukoo na mtala, mtala ni jina tu, kama hivi: Baba ukoo wake ni mvilima, sababu hii watoto wake huitwa Mlakilima wa kike na Kilima wa kiume. Au baba akiwa ni mwenye ukoo wa Walugoma, mtala wa watoto ni Mlalugoma na Lugoma. Kama mama ukoo wake ni Wavilindi, basi watoto wamo katika ukoo wa Wavilindi, akiwa na ukoo wa Wandzeru, watoto ni Wandzeru. Mimi ningefurahi, kama watu wangezoea tena desturi hii ya kuwaita watoto wao kwa mtala, kama Mlakilindi, Mlambena, Mlalukali, Mlamvita upande wa kike, na Kilima, Kilindi, Lugoma, Lukali upande wa kiume. Siku hizi wanaitwa ubinti tu: Binti Abdala, binti Selemani, binti Daudi, binti Lugoma. Upazi unataka kufa, maana watu wanazarau ukale wao. Msiyachukue ovyo majina tu. Mwana mkulu anachukua hata leo jina la baba; baba akifa, kama Mazongela, Kawambwa mshale na majina mengine. Upande wa Undengereko kuna desturi nyingine, Wandengereko huchukua ukoo kwa baba, mtala kwa mama.



Sultani wa Wazaramo ni nani? Watajibu: Hatuna sultani, ila tuna wandewa wengi. Kweli kila mkubwa wa kijiji amejifanya mndewa, hakuna mfalme mmoja tu. Nao wandewa wa kale wamepewa na Pazi Kilama, wailinde nchi. Nao hawakuilinda, ila wamepata kugombana wao kwa wao. Kila mmoja alipenda kuwa mkuu kumpita mwenziwe. Naona, ndivyo vilivyo hata leo, hakuna umoja kwa Wazaramo. Jumbe mmoja kaniambia: Ujumbe wangu mwanzo wake ni ugimbi tu, ndiyo pombe. Nikipika pombe nyingi, watu wananifuata na kunisifu; nisipofanya ngoma, watu hunibeza. Enzi ile wazungu walipofasiri kutoka Bagamoyo, majumbe wakachuma sana, kwani wazungu wale walikuwa matajiri, wametupa feza na baruti na nguo, lakini nyinyi wa siku hizi ni masikini, basi nipe sukari kidogo! Nikamjibu: Siwezi kumpa mfalme zawadi, ni vema mfalme anipe zawadi mimi. Akanyamaza. Huu ndio Usultani?

## Vita za Wazaramo.

Basi Wazaramo wakazama Uzaramo wakakaa, wakijenga miji yao na kulima mashamba yao. Wakapanda muhogo bukini na kizaramo, wakapanda muhindi, mpunga na kunde, chooko na mboga, matango na njugu. Wakapanda na uhemba, ndio mtama, wapate kupika pombe. Lakini shida haikwisha, njaa

zikaingia nchi, kwa hiyo hawakuhesabu miaka, ila wakahesabu zile njaa, kama njaa ya mahimbo, njaa ya nzige, njaa ya panapana, njaa ya kibanga nazi. Miezi yao waliitaja kwa namna yao: Kumosi, kubili, kusatu, kunye, kusano, kutandatu, kufungate, mwinane, mwikenda, mwilongo, seledzi na ndimalala. Nao wahenga wakatia kila mwaka wa nne au wa tano mwezi mwingine, wa kumi na tatu, jina lake masangahu.

Wakavua samaki Ruvu na Rufiji na penye kila ziwa, samaki zao ni dagaa na ndobe na mkunga chui. Wakasaka nguruwe na vinokela, ndio paa wadogo, hata kanga na kololo. Wanacheza ngoma zao za mazunguli na madogoli, za mkole na mbula magutwi na za kulawa, ngoma za wanawake. Walugoma wakachonga ngoma zao, ndio msende na mlungula na muheme na chapuo, mvumi na kingulengule. Lakini hakuna ngoma isiyo na pombe, kweli, kucheza na kunywa kuko pamoja. Walilewa wakapigana kama ilivyo desturi ya popote, asubuhi yake wamesahau yote. Lakini msizani, kama uko utengemano katika nchi ya Uzaramo. Wanagombana ukoo kwa ukoo, mndewa kwa mndewa. Tena utumwa ukastawi vilevile, hii ndiyo hali ya Wazaramo.

Mmezisikia habari za Pazi Mazongela na Pazi Uzimia na Pazi Hembe na Pazi Mlawa, hata za Kawambwa mshale na Ulembo, Mwenesano na Mwinyimgeni, Mwinyiwaziri, na Magombeka, Kibasila na Maruka Mdoe. Siwezi kuwataja wote, kwani ni wengi, walio wandewa wa Wazaramo. Mazongela na Kawambwa mshale walikuwa marafiki sana, kwa hiyo wakasaidiana katika vita za Mafite. Hawa Wamafite wakawasumbua sana Wazaramo mara nyingi, wakiingia nchi kuteka ng'ombe na watu, wakatoka nchi ya Mahenge. Kawambwa akawafukuza mara mbili. Yeye na Mazongela wakawakusanya watu wao karibu ya Sungwi, wakafanya shauri kuwafuata Wamafite katika nchi yao ya Mahenge. Wakawa na selaha zao, hata bunduki na baruti. Wakavaa mikanda yenye pembe, zilizojaa baruti na fataki na risasi, wakajifunza kulenga, wakaenda mpaka Mahenge. Kule wakawanyang'anya Wamafite mali zao, kama wale walivyozoea kutenda Uzaramo. Waliporudi wakasifiwa sana kwa kuwa walikuwa mashujaa. Baadaye Wamafite wakafika Msanga karibu ya Maneromango, ulikuwa labda mwaka wa 1880. Wakachukua hata wake wao na watoto, wakapanga Msanga wakakaa. Tena wakafika Maneromango, wakateka ng'ombe wa Ulembo, labda 50 na mchunga na wanawake wawili. Lakini Kawambwa alikuwapo kwa Ulembo, akawaita watu: wakaja Ulembo na Mwenesano na Chuma na Lukoa. Wote wakawafukuza Wamafite mpaka kwa Muhunzi karibu ya Kisangire. Kule wakapigana Wazaramo na Wamafite, adui wengi wakafa, waliobaki wakakimbia wakarudi kwao. Waliotekwa, ndio yule mchunga na wanawake wawili, wakachukuliwa nao mpaka Mahenge, baada ya miaka minne wakatoroka na kurudi Maneromango tena. Tangu zamani zile Wamafite hawakufika Uzaramo tena. Ila penye vita ya Bushiri walipatana naye, wamsaidie vitani, lakini hawakuweza kitu wakashindwa na Mdachi.



Pazi Hembe alikuwa mwenye nguvu, tumeambiwa, kama amemwua Mfransa, labda mwaka wa 1850, sikupata hakika juu ya habari hii, kwa hiyo siwezi kuwaelezea zaidi. Lakini Hembe na Vumbe mjini Yombo walikuwa marafiki, Hembe alimgawia Vumbe baruti. Siku moja Hembe akamwamkia Vumbe mjini pake Yombo, Hembe akakaribishwa vizuri, Vumbe akaitanda ngozi ya pofu, akamkaribisha rafiki yake. Huyo alipoiona ile ngozi, akatamani kuipata akasema: Nikiondoka, nataka nipate ngozi hii. Vumbe akajibu: Haipatikani, mimi Pazi na wewe Pazi basi, ngozi hupati. Hembe akasema: kama haipatikani,

tutapigana. Basi wakaondokea kupigana, kila mmoja alikuwa na watu wake. Wakapigana kwa bunduki na mikuki, wakafa watu wengi, hata Hembe akapigwa mshale, akafa, mtoto wake anakaa Sofu.

Zamani zile ni karibu ya kuingia wazungu katika Uzaramo. Mwaka wa 1874 akaja Mwingereza, bwana Mekinen, mwenye tembo, akalima barabara kutoka Daresalama kwenda Ruvu na mbele, watu hawakusahau, sababu walikuwa hawajaona tembo wa kufuga, wanaochukua mizigo kama katika nchi ya Wahindi. Wazee wa leo walikuwa vijana siku zile, wakafanya kazi ya kibarua wakapokea kutwa pesa kumi. Baadaye ikapita miaka michache, ndipo wakafika Wadachi, wakapatana na masultani, wakapata nchi ya Uzigua na Nguu na Usagara, baadaye wakafanya mapatano na sultani Sayidi Bargashi, wakapata hata nchi ya pwani, ulikuwa mwaka wa 1885. Waingereza na Wadachi wakapatana kukataza uchuuzi wa watumwa, wakayateka madau yote yaliyopeleka watumwa Unguja na nchi ya Waarabu. Watu wakafurahi, lakini wale wachuuzi wakakasirika, kwani sasa faida yao ilitaka kupotea. Kwa sababu hiyo Waarabu wakafanya fitina wakaangusha vita pwani na mkubwa wao Bushiri. Wengi wakamsaidia, hata Wamafite na makabila mengine walikuwako upande wake. Uzaramo ukajaa vita tena. Kule Pugu wakauawa mapadiri wa Waroma, wasiokosa kitu. Kule Daresalama misioni yetu ilikuwako vita kali, hata dada yake baba Greiner akapata risasi mkononi, nao watoto waliokuwa wamekombolewa katika utumwa na serikali na kukaa misioni, wakapata shida, wengine wakatekwa, wengine wakapona. Lakini Bushiri hakuwaweza Wadachi, mwisho akashindwa karibu ya Bagamoyo. Ukitaka kukumbuka vema habari hizo, siku utakapofika Bagamoyo, uwaombe watu wa kule, wakuonyeshe jiwe lile la ukumbusho karibu ya boma. Penye jiwe lile yameandikwa majina ya



wote, waliokufa vitani siku zile upande wa Wadachi. Bwana Hambaroni na bwana Wismani walikuwa wakubwa siku zile, nao walimshinda Bushiri na kulivunja boma lake karibu ya Bagamoyo. Bushiri mwenyewe akakimbilia Uzigua, lakini watu wa kule wakamtoa mikononi mwa Wadachi, akapelekwa Bagamoyo akapigwa risasi au akanyongwa. Sasa Wazaramo wakapata utengemano. Hayo yote yalifanyika mwaka wa 1887 mpaka wa 1891.

Baada ya miaka 15, ndio mwaka wa 1905 na 1906, ikaingia tena vita, ndiyo vita ya majimaji au Wazaramo wanavyosema: Vita ya Kalava dikono. Waislamu na wakubwa wa nchi pamoja na waganga wakafanya fitina kule Lindi na nchi ya Wangindo na ya Wamatumbi. Waganga wakatangaza hivi: Mungu Koleo anawakataza watu kuwatii Wazungu na kuwapa kodi, sababu hii muwafukuze Wadachi, bunduki zao zitatoa maji tu, wala si risasi, anayekunywa dawa, hatakufa vitani, atapona. Hata Uzaramo ukaingiwa na matata hayo. Waganga wa Wamatumbi wakaingia nchi ya Rufiji na Kisangire, wakawachochea watu maneno na kuwapa dawa ile. Kila mtu akalipa kodi pesa mbili, ndiyo kodi ya Koleo. Sababu hii, mungu yule akaitwa mpaka leo: Mungu wa pesa mbili. Lakini mganga akamwambia Kibasira: Baba yako amesema nami kutoka kaburini mwake, akatoa mkono na kusema: Msimpe Mdachi kodi. Kuonekana hakuonekana, ijapokuwa mganga alisema: Kila atakayefika Kisangire atamwona mungu. Basi hata leo Wazaramo husema: Kalava dikono, maana yake: Mungu ametoa mkono tu, mwenyewe hakuonekana. Wajinga walikuwa wakisadiki maneno ya mganga, wakajitia katika shauri lile baya, wakapigana na Mdachi, lakini wakashindwa, kwani bunduki hazitoki maji, ila risasi kweli zikatoka katika bunduki za askari, watu wakafa wengi kwa ujinga wao. Kibasira akakimbia, lakini rafiki zake

wenyewe wakamtia mikononi mwa Mdachi, akanyongwa. Nao watu wakapewa amri kumwangukia Mdachi. Nimeona mwenyewe, walivyokuja Maneromango na ngoma zao, wakiimba: Tunataka kumwangukia bwana mkubwa. Wakapata amri ya kujenga karibu ya njiani, wasijenge porini, walivyozoea kila siku, wakakubali. Baada ya mwaka nchi ikatulia, lakini enzi ya Kalava dikono hatujaisahau, nao watu waliokuwamo katika fitina ile, leo wanakana, kwani huona soni, walivyodanganywa na waganga wao.

Vita hizi zote si kitu, tukizilinganisha na vita ya mwisho, vita hii kubwa, iliyokuwa vita ya miaka mine. Lo, ilikuwa shida kubwa na machafuko mengi, nani anayeweza kusahau wakati huo? Nao Wazaramo walikuwa vilevile katika uaskari na upagazi na vibarua, waume na wake wakasumbuka sana. Wengi wamekufa vitani, wengi wamekufa kwa marazi. Sitaki kuwaandikia hayo yote, kwani mmeyajua wenyewe. Iila nasema tu: Mungu ametuopoa katika shida hii yote, yeye ameonekana mwenyi rehema, nao watu wameonekana wenyi uchukivu mwingi. Sasa Mdachi ameshindwa, na nchi inatawaliwa na Mwingereza, yeye anawasaidia sasa watu wa Tanganyika Territory, basi tumtii yeye, hata sisi Wazaramo. Na wandewa wa Wazaramo ni wandewa chini ya serikali yao Waingereza, nguvu inatoka kwa serikali. Kila mtu na autii ukuu! Maana uko na nguvu kumpita yeye. Kwani hakuna ukuu usiotoka kwa Mungu. Nao wote ulioko umewekwa na Mungu.

## Tabia na desturi za Wazaramo.

Wenzangu, ningalitaka kuandika yote, ingenipasa kuandika kitabu kizima na kikubwa, lakini nitawakumbusha kidogo tu, watoto wenu waone hamu ya kuwauliza wazee wao habari nyingine. Tabia na desturi za Wazaramo zimechanganyika na mambo



mengi yaliyotoka kwa makabila mengi. Upazi safi hauko enzi hii. Masimulizi yenu ya Upazi yako hata leo, ndiyo masimulizi ya wanyama, walio kama waana Adamu, kama masimulizi ya kibarabara na simba au ya dudumizi na sungura, au ya jogoo na sungura au mengine kama haya. Lakini ukiyasikia masimulizi ya watu na Mungu au ya masikini na tajiri au ya malaika, ujue kama si masimulizi ya kipazi ila ya Waswaheli na ya Waarabu. Upazi na Uswaheli umechanganyika. Hata ukisikia mifano na vitendawili, utatambua, vilivyo vya Upazi na vilivyo vya Uswaheli. Wabili hawaga ndzila, maana yake: Wawili hawapotei njia. Seke ukalalile kuugwile, seke ukalalile kwikwangwale, maana yake; usipakasirikie ulipoangukia, usipakasirikie ulipojikwaa. Si mifano ya kizaramo? Lakini ukisikia maneno kama hayo: Haba na haba hujaza kibaba au: Haraka haraka haina mbaraka, utajua, kama ni ya Waswaheli.

Ninafurahi kila mara, ninaposikia masimulizi ya kuwaonya watoto, wawaheshimu wazee. Vijana wanaonywa kuwatogola wakubwa na wazee. Hawana ruhusa kuwaamkia wazee kama hivi: Kwa mgima gwe, ila: Mwa wagima mwe. Usimwambie mzee: Hujambo, ila: Hamjambo? Mtoto asimngoje mkubwa amwamkie kwanza, ila mtoto atangulie kuwaamkia wakubwa. Tena watoto huwaheshimu wazazi wao, baba na mama. Mtu asimtukane baba au mama ya mwenziwe, kwani atapata matata, kwani watapigana. Naona, kweli yafaa kuwatii na kuwaheshimu wazee na wakubwa, ndivyo alivyoagiza hata Mungu katika agizo lake la nne. Wazaramo husema: Kukula bule kulawa mgongo. Maana yake: Umekua bure na kutoka mgongoni pa mama, hukulipa kitu. Nimewaona vijana wa leo wameacha kidogo desturi hii ya upazi, inafaa wajizoeze tena walivyozoea vijana wa zamani. Basi usimzarau mama, aliyekulea bure. Akili ni kwa walala, inafaa kusikia mashauri yao.

Hujazidiwa; ukizidiwa, kwa mjomba utakwenda kweli asiyemjua mjomba, siku za taabu atamjua na kwenda kwake amwombe msaada.

Cha mguhi kimalile mwiti, maana yake: Aliye mfupi, mali itamwisha kichwani. Lakini huu ni mfano tu, maana ya kweli ni hii: Aliye peke yake, labda hana ukoo mkubwa, watu watamdanganya, kwani hana nguvu. Nguvu ya mtu ni ukoo mkubwa, unaomgombea mtu wake. Watu wa ukoo mmoja ni kama watu wa usharika mmoja, wanasaidiana katika maneno yote, mmoja wa ukoo akitingwa, wenziwe watamkomboa. Mjomba au mkolo ni mkubwa wa ukoo, anayetengeneza mashauri ya ukoo, nao watu wake wa ukoo watamsikia sana. Shauri la kuoa au kujenga nyumba au la kulima ni kwake mjomba, ndilo shauri la kaka yake mama. Hapo tunaona, Wazaramo wanavyoweza kukaa kwa umoja. Si vema hivi? Nyinyi Wazaramo mwikumbuke desturi hii, hata mkiwapo katika ugeni, mjue nyinyi ni wa ukoo fulani, watu wenu huwapenda. Siku za shida mkumbuke: Ukoo wenu utawakomboa. Nimejua, ya kuwa hata ugomvi mwingi umo katika ukoo mmoja, lakini watu wanajaribu kupatana vema, na ukoo mmoja ni kama nyumba moja, ni undugu. Ni vema, ndugu wakikaa pamoja na kupatana.

Hata utani au kwa Kizaramo ugongo ni desturi njema; watu wa ukoo mmoja hufanya utani na ukoo mwingine, maana wasaidiane katika kuzika. Wagongo ndio wanaozika, mgongo huwasimamia wale wanaozika, nao huwatii kila neno siku ya maziko. Wagongo husharikiana hata katika chakula na mali. Mgongo akichinja kuku wa mgongo mwenziwe, si wizi. Pazi si urafiki wa kweli?

Kila siku ninaposikia watu wanapoamkiana: Jambo? Nasikitika, kwani „Jambo“, neno hili halina maana zaidi. Wazaramo wana namna nyingine za kuamkiana, mbona huacha namna hizi? Kwema ukaye? au: Kwa mgima? Na mgima? au: Kazi mafundi? Awali Mungu! Au: Konde? Ya kuwasa, ya baho! Au kumwamkia mwinda nyama: Nhanzi? Majibu: Ya nyama, au: Ya bule! Ya tosha, tumeona, Wazaramo walivyo na namna nyingi za kuamkiana, inafaa mtumie vile, walivyotumia wahenga wenu.



Lakini Wazaramo wamezoea kunywa pombe, ndio ugimbi, sababu hii wengi ni walevi, wanapoteza akili. Husema: Pombe ni chakula chetu, hatuwezi kuacha. Ndio, huwezi kuacha, lakini usilewe, kwani ugomvi na matata mwanzo wake ni pombe tu. Nikiwaona watu waliolewa, siwezi kuongea nao, kwani hawaangalii maneno yao, akili yao imegeuka. Wakijenga nyumba, ni kwa pombe, pombe ya kulimia, wanakata nyasi kwa pombe, wanatambika kwa pombe, hata kupunga pepo na pombe, jando na pombe, lo pombe ni bora kwao Wazaramo, wala hawajui wanavyoharibiwa na pombe, hawawezi kusaidiana pasipo pombe. Ingenipasa kuziandika habari za wanawali, wanavyokaa nyumbani mwaka mzima na zaidi, na habari za kuoa na kuzika, lakini nimeona, ya kuwa desturi za Wazaramo na dini yao huchanganyika, hazitengeki. Kwa sababu hii naongea nanyi habari za dini yenu.

## Dini za Wazaramo.

Watu wa namna mbili walio na nguvu ndio wanaotawala Wazaramo. Mnazani, ni wandewa na majumbe, lakini sivyo, ni waganga na wachawi. Hawa ni mafundi, nao watu wote wanawatumaini waganga na kuwaogopa wachawi. Watu husema: Mchawi ndiye mtu mbaya, anayewaloga watu tu, anapenda kuwaumiza watu; mganga ndiye anayejua kila dawa, anawaagua watu, awaponye. Lakini mimi nasema: Mganga ndiye anayezila feza za watu, Mungu anawaponya. Waganga wanajua kweli

dawa zinazofaa, kama majani ya miti au mizizi yake au mbegu na jivu, dawa hizo zinafaa kwa magonjwa mengi. Watu husema: Sisi tunatumia dawa ya kiswaheli, inatuponya. Mara nyingi inamponya mtu, sababu hii si vibaya kuzitumia dawa hizo. Lakini mganga atasema vilevile: Sina budi hata kupunga pepo, kwani yeye ameleta ugonjwa, au sina budi kutambika, mizimu ipoe kwanza. Kila pepo ina mganga wake, kuna waganga wa kinyamkela, wa mizuka, wa majini, wa kila namna. Mganga anayo hata dawa ya kuharibu uchawi, anavyosema yeye. Watu hutegemea, ya kuwa waganga na wachawi ni wenyi nguvu ya siri, isiyo nguvu ya kimtu, ila ya shetani au ya miungu. Wanaweza kuanga na kugeuka simba, wanalagula na kuzinga nyama, ni vioja vikubwa, sababu hii watu huwaogopa sana. Unaweza kuwafahamu waganga, ukiona mkoba wao wa bwenzi kichwani. Hata mambo ya dini yoyote wanajua.

Wazaramo huzani, kama dunia imejaa pepo za kila namna, pepo hawa ni kama watumishi wa Mungu. Lakini mwanzo wa pepo ni wafu au kivuli cha wafu. Kila nyumba ina kungu zake, ndiyo mizimu, naye mzee wa nyumba anawatambikia. Ngoma ya mazunguli ni kama ibada ya wamizimu, tambiko lao ni pombe na togwa. Siku nyingine hutambika tu, wakipatwa na taabu, kama ugonjwa au njaa. Huomba hivi: Tukugalile wandzukulu dzako, uwagolelele upile! Au wakifanya safari, huomba: Mwanza wangu nihongolele goya, sikunyugulege. Hujenga kibanda penyi kaburi, huweka tambiko lao juu ya kaburi. Hutumaini, kama tambiko litawapoza kungu au mizimu, wao waondoe shida zao.

Basi wale kungu naona hugeuka baadaye, huwa mazezeta, ndiyo pepo za wafu wote, za kila ukoo. Nao hupelekewa vilevile tambiko. Vinyamkela ni pepo za watoto, mizuka ni pepo za watu waliokufa



pwani, majini ni pepo za wauaji na watu wabaya. Hawa wote huwaingilia watu na kuwapa ugonjwa, hivi watu hupagawa na pepo. Kwa sababu hii hawana budi kufukuzwa au kupungwa, wagonjwa wapone. Nyinyi nyote mmejua mhungi au madogoli, waganga wanavyopunga na kutetema. Wanasumbuka usiku kucha, mpaka mzuka anaposema na msemo mwingine, ndio anamtoka mgonjwa. Je, si woga mtupu, unaowashika Wazaramo? Hawasemi, kama wale pepo ni miungu, lakini wanawafanya kama miungu yao, wanawaogopa sana. Kama wangalikatazwa na serikali desturi hii ya pungi, wangekasirika sana na kusema: Tukikatazwa kupunga, atakayeponya wagonjwa wetu ni nani?

Basi, sasa tufikiri habari za Koleo. Pazi Kilama alipotoka Kutu, alileta hata habari hii ya Koleo. Ikaingia Uzaramo, inashikwa na watu hata leo. Ukoo wake Koleo ni Wamlali, wanaokaa Kutu hata leo, Mlamlali ni mtambikaji wake Koleo. Konde anakaa Kambangwa kuwa mtumishi wa Koleo. Koleo huleta mvua, ndivyo wanavyosema watu. Hata Walugulu hutegemea hivi, huenda kwa Kingalu kumpa mbuzi, aombe mvua. Hata Kambangwa hana budi kwenda Uluguru, akitaka kuomba mvua kwa Koleo. Je, Koleo ni pepo ya mtu wa zamani? Wanasema, kama anakaa katika pango, mle pangoni mna maji, yanayovuma, ndiyo sauti ya Koleo, watu huona ni kweli Koleo anayesema. Mmesoma habari ya mungu wa pesa mbili, ndiye huyo huyo. Hata wakati wa mavuno pengine hutokea mganga husema: Haya jengeni changa cha mulungu, mavuno yasafike. Msipojenga na mkila ovyo tu mavuno, mtapata magonjwa! Watu wanajenga vyanga vya mulungu, wanazima moto wote nyumbani mwao, wanapekecha moto vyangani na kukanga uhemba wa kwanza, ndio mtama, wanakula. Nao wanawake huchukua moto mpya mle vyangani, wapeleke nyu-

mbani. Ndivyo wanavyoyasafisha mavuno yao na baadaye huvuna. Sijui, kama hivi wanamkumbuka Mungu wa kweli au wanamtambikia Koleo.

Pana mizuka ya kila namna, kama kibwengo, tali, dungu malo, mulugulu, seng'ombe, simba na wengine wengine. Pana mwenembago, lo, Wazaramo hawapati raha, hawapati kutengemana na kutulia sababu ya „zimbeho". Tena wana mwiko wao, wauangalie, wasile, wasipate ugonjwa. Wana dawa ya lutego, wezi waogope kuiba vyakula shambani mwa watu. Wanamwogopa kila mgeni, kwamba labda ni mchawi. Wakizaliwa mapacha, ni kibi, wanawaogopa, kwani labda huleta shida, zamani wamemtuma mmoja wao mapacha au kuwaua wote wawili; au mtoto akipata kwanza meno ya juu, ni kibi; au mtoto akizaliwa vibaya, ni kibi, asilelewe, inafaa atupwe. Basi si masikini na wapotevu?

Zamani sana hata dini ingine imeingia katika nchi, ndiyo dini ya Uislamu. Dini hii imeleta na pepo nyingine, kwani majini na mizuka ni pepo za waislamu. Dini hii imeyabadili mambo mengi katika nchi, zamani watu hawakujua habari za jando; ila vijana walikua, „kukula" wanasema Wazaramo, chini ya mti mpingo wakafanya ng'hula yao, wakafundishwa utaratibu wa kipazi, wakapewa jina la ukubwa, hawakutahiriwa. Siku hizi vijana wengi huingia kumbini, hutahiriwa, kwani leo wanaona soni wasipotahiriwa. Je, wahenga wenu waliona soni? hawakuzaa watoto vilevile? Mimi naona, uislamu haukutoka Daresalama au Bagamoyo, ila umeingia katika nchi kutoka kusini kwa Wangindo, waliopatana sana na Waarabu enzi ya utumwa. Sababu hii kusini kwa Uzaramo waislamu wamezidi penye Ruvu; lakini haukufika zamani, ila enzi ya leo. Hata leo utaona ngoma ya ng'hula huchezwa Ruvu. Uislamu ulileta uharibifu kwa Wazaramo, hauonekani waziwazi. Wazaramo husema: Uislamu umetuletea



faida, kwani ulitutoa katika ushenzi, tumegeuka kuwa Waswaheli sasa. Hawafikiri maana ya dini hii, wamesahau shida ya utumwa, hawatambui, jinsi tabia zao zilivyoharibika.

Mimi sitaki kusema mengi. Uislamu umefundisha nusu ya kweli, kama kuna mungu mmoja tu, aliyeziumba mbingu na nchi. Wahenga wa Wazaramo nao wametegemea kuwa kuna Mungu, aliyeumba mbingu na nchi, watumishi wake ni wale pepo. Uislamu hufundisha hata kiyama, wafu watafufuka, mwisho, wabaya watahukumiwa, wema ndio waislamu, wataingia peponi, Isa Masiya atarudi kuwahukumu watu. Lakini nani, walio wema na wabaya? Hapo wanapotea wengi, wanajidanganya wenyewe wakisema: Wema ni wale wanaofunga Ramazani na kukataa nyama ya nguruwe, wanaosali, waliosilimshwa. Kuna mtu duniani asiyekosa? Je, nani basi atakayepona barazani pake Mungu? Nani atakayeweza kusema siku ile ya hukumu: Bwana, mimi nilifunga, nilikataa nyama ya nguruwe, sikufanya yaliyo haramu! Bwana Yesu atauliza: Je, uliwapenda ndugu? Uliwasaidia wenye shida? Ndipo tutakaposhindwa kujibu. La, wema wetu hautatuponya, kwani tumekosa mengi. Tukitaka kupatanishwa na Mungu, lazima tupate mtu aliye mwema kweli, yeye atupatanishe na Mungu, tuondolewe makosa yetu. Lakini hayo atayatambua mtu yule tu, anayefahamu habari za Ukristo. Sababu hii naona hatari kwa Wazaramo, watu wakisilimshwa na kushika Uislamu. Wazaramo walipata nini? Wengi wao ni waislamu, lakini hutambika vilevile, huogopa uchawi, hupunga mizuka na kinyamkela na majini. Lakini hawawezi kumpenda yule Mungu mmoja. Waalimu wao wamepata kuwa waganga wao. Pale wanapokuwa na neno, huenda kwa jumbe huhukumiwa kwa sheria ya kipazi? Sivyo, ila kwa sheria ya Waarabu, sheria ya msahafu. Zamani „wadja

sale“, leo hupiga amini, zamani wamekua kwa „ng'hula“, leo wanaingia jando, zamani walikuwa Wapazi, leo ni Waswaheli. Hujivuna: Tumetoka katika ushenzi, hubeza kabila yao na tabia zao. Wameacha pombe? Zamani wameoa „mwelie“, leo wanachukua mchumba tu, kusudi wapate kumtupa, kila wanapochoka. Tamaa zao zimepunguka? Je, wanawake wamepata ruhusa ya kutambika au kusali? Sitaki kuwaandikia mengi juu ya habari hii ya dini hii, mfikiri vema faida au hasara ya mambo hayo, kama Wazaramo wamepata kutengemana rohoni mwao au sivyo, kama wamestawi zaidi au sivyo. Naona, dini maana yake kutuliza roho ya mtu, apate kuishi na kufa kwa utengemano. Nasikia, wanavyosema: Je, tufuate Wazungu na dini ya kizungu? Wenzangu, kweli Wazungu walipoingia katika nchi yenu, ikaanza enzi mpya kabisa, tena yameingia mambo mengi, yanayowafaa watu wa Afrika na kuwafaa hata Wazaramo. Nyinyi nyote siku zote mnatumia vitu vya kizungu, vibiriti na nguo, vyombo vingi na mali nyingi, mnakaa na raha nyumbani na katika nchi yenu. Pazi Kilama angaliweza kuona haya, angestaajabu, lakini naye angeona utamu wa vitu vya kizungu, kama alivyoona utamu wa chumvi zamani. Vita ya nyinyi kwa nyinyi imekwisha, utumwa umekoma, uchawi ukionekana unaazibiwa; mali imezidi katika nchi. Njaa ikitaka kuingia katika nchi, watu watasaidiwa; dunia imegeuka kweli, wala hamuwezi kulibisha neno hili, ni kweli. Lakini pamoja na Wazungu wameingia hata wamisionari wanaotangazia watu dini mpya, wala si dini, ila wanatangaza habari ya mwokozi mwingine ndiye Yesu Kristo, yule yule Isa Masiya.

## Misioni katika Uzaramo.

Hata Uzaramo wameingia waalimu wa kizungu tangu ilipoingia enzi ya kizungu. Mwaka wa 1887



akafika baba bwana Greiner Daresalama, akaanza kazi ya misioni kule Daresalama na Uzaramo. Sisi sote tunalijua kaburi lake karibu ya kanisa letu la Kiserawe. Kabla hajafika, watu walisema: Atakuja mtu malaika, atakayetengeneza yote Uzaramo. Basi walipomwona baba Greiner, wakasema: Huyu ndiye, atakayetengeneza yote. Alipokwisha fika akajenga nyumba ya misioni kivukoni Daresalama. Serikali ilikuwa ikiwakomboa watumwa; waliokuwa wakubwa, wakapewa ruhusa kwenda kwao, waliokuwa watoto na vijana wakapelekwa misioni. Hata baba Greiner akapata watoto, akawapokea vizuri, awalee na kuwafundisha. Kwanza Daresalama, baadaye tangu mwaka wa 1892 akajenga hata Kiserawe na kuweka wengine kule, waume na wanawake. Akapata na wasaidia, kina baba Wohlrab na Gleiss, hata baba Beye na Masi na wengine wengi, kama baba Kenisi na Wenzeli na baba Kilamroti na wengine, tunaowajua. Wote wakafanya kazi ya misioni. Hata wagonjwa wa kizungu wakasaidiwa kwanza Unguja, baadaye Daresalama misioni, mpaka serikali ilipojenga hospitali ile kubwa kwa Wazungu na hospitali ya Sewa-Haji kwa Waswaheli. Wazaramo waliona ile misioni na kazi yake. Waliweza kulinganisha na kazi zote nyingine, kama kazi gani inayowafaa watu. Wengine hata leo wako wazima, waliomsaidia baba Greiner kujenga nyumba zake, wakapokea mshahara wao, wakaona, alivyowachunga vema watoto na kuwatunza. Mzee mmoja aliniambia neno hili: Baba Greiner ametuponya katika vita vya Bushiri ametusaidia katika shida ile ya siku zile. Wale watoto, waliotoka utumwani, wako wapi? Wengi labda wamesahau mema yote waliopokea misioni, kama wasingepelekwa misioni siku zile, wangalipotea kweli. Wengine walifundishwa useremala au kazi ya mwalimu au kazi ya uwashi, wakapata kazi njema na mshahara mwema. Wakati wa njaa pana-

pana wakashiba misioni. Kila anayetaka kuona anaona, misioni ilivyofanya vema, wala haikufikiri faida. Lakini ilivyo dunia hii, Wazaramo husema: „Mulungwana na midevuyo, mkele wamulile" au: „Mkanda keha, ziyembe zinoga". Maana yake: hela na chakula cha misioni ni kizuri, lakini waliotugawia mema tunawakataa.

Enzi ile ya vita yake Bushiri, baba Greiner hakuwafukuza watoto, wala hakukimbia mwenyewe, awaache wakiwa, ila akawatunza vema watu wake. Tumesikia, vita ilivyokuwa kali pale misioni, maadui wakawateka watoto wengine, lakini wengi wakapona. Vita ilipokwisha, Bushiri aliposhindwa, baba Greiner hakuchoka, akaendelea kujenga na kuchunga watoto. Nimeambiwa na mtu, aliyefanya kazi kwake: „Kila asubuhi waliingia kanisani, wakasikia masimulizi ya wazungu, lakini sisi vibarua hatukuingia tukasema: Si kazi yetu kuomba kizungu, lakini baba Greiner hakutubeza, akatutunza vilevile." Naye aliyeniambia maneno haya, yuko mzee siku hizi, amekubali masimulizi ya kizungu, amepata kuwa mkristo, amejua sasa, ya kuwa si dini ya kizungu, ila dini ya watu wote. Mwanzo wa kugeuka kwake yule mzee ni kule Daresalama kwa baba Greiner. Sisi tumefahamu, ya kuwa si baba Greiner, wala si mwalimu wowote wa kizungu, ila ndiye Bwana Yesu, aliyefika pwani na Uzaramo. Wamisionari walitangaza tu: „Msiogope! Kwani tazameni, tunawapigia mbiu njema yenye furaha kubwa itakayowajia watu wote. Kwani mmezaliwa Mwokozi wenu, ndiye Bwana Kristo. Yeye anapenda kutengeneza nchi yote, watu watengemane. Nao watu wakaonja utamu wa neno hili. Wengi wakalishika, wakapata kuwa wakristo.

Lakini kule Daresalama si Wazaramo tu, ila kila kabila, kule kuna mambo mengi, yanayotia tamaa, watu wasifikiri kutaka dini tu, sababu hii ni wachache tu, walio wakristo wanaofuata shauri hilo la



Mwokozi wetu. Kuna Wanyasa, Wanyamwezi, Wasukuma, Wabena, Wahehe na makabila mengine, kuna askari na maboi na makarani na waalimu na vibarua, watu wa kila kazi. Nao wakristo wa bara huja Daresalama, hufika hata misioni. Tuna kanisa kule K. A. R., hata kule Kaliyakoo, tunatumia hata kanisa la Wadachi mjini. Ng'ambo tuna shamba la minazi, misioni ipate faida kidogo kwa kazi ya misioni. Huko ng'ambo kuna shule kwa watoto wa ng'ambo, nao Wakristo na wanafunzi hukusanyika mle shule kwa kuomba. Mchungaji Martin Ganisya huwachunga vema, akisaidiwa na waalimu na wazee wa kanisa, nao hufanya bidii ya kuwatunza wakristo wa pwani. Aa, pana kazi nyingi za misioni, na watu wa kila kabila wanaweza kusikia neno la Mungu. Wakristo wa kila misioni ya kievangelishe waliomo mjini husharikiana kwetu Daresalama. Hivi kazi ya misioni inastawi, usharika wetu unaenea pwani pale, walipokaa zamani Wamashomvi katika kijiji kile cha Mzizima.

Zamani tangu baba Greiner alipoingia nchi hii, ndugu zetu wa misioni ya Beteli walishika kazi hii ya Uzaramo, inafaa mkisoma habari yake bwana Pastor von Bodelschwingh, aliyetunza zamani misioni hii. Yeye aliwaonea huruma watoto wa utumwa, akawasaidia sana. Mwaka wa 1903 misioni inayoitwa misioni ya Berolina ikapokea kazi hii ya Uzaramo, naye baba Kilamroti, mnayemjua nyinyi nyote, alivyoanza kazi, alivyoitwa na Mungu vitani na kuzikwa Daresalama, penye makaburi ya Wadachi yaliyo pwani. Sitaki kuwataja wamisionari wote, kwani nyinyi mnawajua, walivyokaa katika yenu, nami nisimsahau mmoja, asije akahuzunika. Kila mmoja amefanya kazi kwa uwezo wake aliopewa na Mungu.

Mwaka wa 1892 baba Greiner akaanza kazi Kiserawe, watoto wengine wa utumwa walipelekwa Lutindi Sambaani, wengine wakahamia Kiserawe,

wakakaa huko. Shule nyingi zikafunguliwa, hata Mitelshule ikafunguliwa Kiserawe. Watoto wakapata kuzidi akili. Nao Wazaramo wakaanza kusikia ule utume mwema. Wakati ule ikaingia njaa kali ya panapana, mwaka wa 1898 na 1899 watu wengi wakafa kwa njaa, wengi wakafika misioni wakaomba chakula, wakalishwa na kufundishwa. Enzi ile ya shida Wazaramo wengi wakageuka roho na kubatizwa. Kiserawe ukastawi vizuri sana. Baadaye njaa ilipokwisha, watu wakapunguka misioni, wengine wakarudia nyuma, wakamsahau Mungu. Nilipofika mimi, mwaka wa 1904, Wadachi wakaanza kujenga reli kutoka Daresalama kwenda mpaka Kigoma. Lo, kila aliyejua kazi kidogo ya ufundi, akafuata kazi penye reli, hata mafundi wa misioni wakatuacha, wakayafuata mapesa kwenye reli. Wengine hawakuonekana tena misioni, sijui, kama wazima bado ama wamekufa. Leo tumezoea reli na motokaa. Walio na shilingi moja, au mbili, hawaendi tena kwa miguu, huingia mashine au motokaa, wengine wananunua motokaa ya kiswaheli, ndio baisikeli, wasafiri hivyo. Ukiwa na feza, haya uingie motokaa, lakini usikope! Basi, nawasimulia habari hizo tu, sababu tangu enzi hii kazi ya Kiserawe imerudi nyuma, wale wakristo wake ni wachache leo. Nao wasichoke kuwa waelekevu, kwani Mungu hawezi kuwasahau watu wake. Mwinyiwaziri na Pazi Uzumia na Seremani na Magombeka, nao wote wa Kiserawe, nao wasisahau mema, waliyopewa misioni.

Misioni ya tatu ya Uzaramo ni Maneromango, ilianzwa mwaka wa 1895. Baba Greiner ndiye aliyeanza kule, akafanya safari yake kufika Konde, akapatana na yule mzee Ulembo, baba yake Ulembo wa leo. Wakajenga misioni, bwana Masi ndiye aliyejenga, akaanza kazi ya misioni Maneromango. Enzi ya panapana watu wa kule wakapewa chakula kwa kazi ya mawe, wakatuta mawe kwa kujenga nyumba



ile kubwa, wakapokea mchele au chakula kingine, hivi wazungu wa misioni na Wazaramo wakasaidiana. Watu walikubali neno la Mungu kule Maneromango tangu mwanzo, wengine wengine wakaja kuomba mafundisho, mwisho wakabatizwa. Nilipofika mimi safari ya kwanza Maneromango, nikawakuta wakristo 50 au 70, leo wako zaidi ya 600. Baba Worms, aliyezikwa karibu ya kanisa, alikuwa na bidii sana, akatembea sana akihubiri kwa kizaramo na kufundisha kwa kizaramo. Watoto wengine wa Maneromango wakapelekwa Kiserawe Mitelshule, waendelee zaidi. Lakini Uislamu ulianza kuingia kule vilevile, ukawazuia wengi kulifuata neno la Bwana wetu Yesu, hii ni huzuni yetu. Hata wakristo wengine wameacha ukristo wao, wakasilimshwa sababu ya tamaa tu. Inafaa wakiturudia, wasipate kupotea. Mmoja katika hawa walikuwa wakristo zamani na baadaye kuishika dini ya Muhamadi, amesema: „Mbona nashiba hata sasa, mbona Mungu ananipa riziki, mimi niliyemwacha Mungu wa kikristo nikachukua wanawake wengine? Basi, Mungu amekubali.“ Je, enzi ya kesho, huyu asione alivyopotea.

Enzi ya Kalava Dikono misioni imewasaidia watu, Akida Mwinyimbegu aliposhambuliwa na watu wa Mfulu. Wao walimjia Mwinyimbegu kumkomboa mzee wao, alikuwa amekamatwa na Akida na kufungwa sababu hakulipa kodi, ila alichanga kodi ya Koleo, kichwa pesa mbili. Basi, walipomuopoa mzee, Akida akakimbia Daresalama na wakewe na mali na kodi ya serikali, sisi tukakaa peke yetu misioni, hatukukimbia. Bwana shauri akaja na askari wake na mkalimani wake Osmani, watulize nchi. Lakini siku moja Osmani akarudi kutoka Msanga, alikuwa amepigwa risasi njiani na Wazaramo wa kule, akafa nyumbani mwa misioni, akazikwa pale misioni, kaburi lake liko hata leo. Pale bwana shauri akajua, kweli vita, akaondoka akapigana na maadui. La-

kini akaja bwana Hauptmann Fonk na kompania yake, akapokea kazi ya bwana shauri, akapigana na wale maadui, akatuliza nchi. Watu wakaangukia wakatambua ujinga wao. Mndewa Ulembo alikuwa upande wetu. Maadui hawakumwambia kule Msanga: „wewe Ulembo, ufike mbinguni pamoja na wazungu wako, lakini usionekane hapa duniani?" Lakini waliofuata shauri la misioni, hawakupata hasara hata kidogo. Hivyo vita ya majimaji ikaisha, nchi ikatengemana tena, kazi ya misioni ikaendelea vema. Kazi ingine ya misioni ni kuwauguza wagonjwa, tangu mwanzo watu elfu elfu wamepata dawa misioni Maneromango, dawa ya ubovu, dawa ya safura, dawa ya homa, dawa zozote. Wagonjwa wanatoka mbali, kama Bagamoyo na Ruvu na Kisangire, wakapata dawa. Leo wako mama wawili, mmoja hutunza wagonjwa, mmoja hulea waanawali. Ukitaka kuona mambo hayo, nenda misioni Maneromango, uone! Haya yote, sababu yake ni nini? Ni sababu ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwani kwa agizo lake tumo Uzaramo, upendo wake uonekane waziwazi, watu wapate kumfuata yeye.

Kuna kazi nyingine kule, kazi ya ufundi; viti vya Maneromango vimejulikana mpaka Nairobi na Mwanza na Kigoma. Sanamu zinazochongwa vilevile zimeenea. Faida ya kazi hii si ya misioni, ila ya watenda kazi hii, ndio Wazaramo. Nao watoto wangapi, waliofundishwa shule, wangapi, waliosaidiwa katika shida zozote? Mimi nimejua haya, kwani nimekaa mwenyewe Maneromango tangu mwaka 1905, nimejua kila jambo la pale misioni. Nimesharikiana nanyi katika shida na furaha, shida ya vita na furaha ya katika usharika wa wakristo. Yesu huwaita Wazaramo: „Njooni kwangu nyote, wenye kusumbuka na wenye kulemewa na mizigo! Nami nitawatuliza." Yeye Yesu anapenda kutengeneza mambo yote ya Uzaramo.



Lakini kazi ya misioni ilikuwa katika hatari kubwa wakati wa vita kubwa, wamisionari wa kidachi walipopelekwa kwao. Hapo waislamu na wamizimu wakaanza kucheka na kuwabeza wakristo: „Yuko wapi Mungu wenu? Ameshindwa, waalimu wenu hawatarudi tena, basi mgeuke, mtufuate sisi!" Kweli tulihuzunika, tukazani, ya kama huu ni mwisho wa kazi yetu. Lakini Mungu hakutusahau, ila akasikia kuomba kwetu sisi sote, wamisionari wakapata kurudi. Tangu mwaka wa 1926 kazi ya misioni Uzaramo ikapata waalimu wake wa kizungu tena, nao wakristo wakaongezeka. Pazi Kilama alipokwenda vitani, watu wengi wakaenda naye, hata Wakutu. Lakini Pazi hakujua kazi ya hesabu ya askari wake, akaweka ngozi njiani, nao askari wakakanyaga ile ngozi ya ng'ombe safari ya kupita njiani, basi walipokwisha pita, ngozi ikatoboka kwa uwingi wa watu waliopita na kuikanyaga. Sasa mfalme wetu Yesu Kristo anapiga vita yake Uzaramo, hesabu ya watu wake inazidi; ingefaa wakizidi sana, tushindwe kuwahesabu walio askari wake. Lakini inafaa na nguvu yao izidi, Satani asiharibu nchi na watu wa Uzaramo.

Zamani zile za Pazi Kilama zimekwisha pita, nchi ni mpya kabisa, mambo mengi yameingia duniani; Wapazi hawana mfalme wa umoja, hawana kiongozi, anayefaa, awaongoze katika enzi hii ya mambo leo. Basi ingefaa wamkubali mfalme wa mbinguni. Dini ya Upazi inaanza kuchakaa, si sababu ya misioni tu, ila sababu ya mambo leo, sababu ya kuchuma na kuhemea huko na huko. Mtu mmoja wa kiafrika aliandika hivi: „Nguvu ya feza inazidi leo Afrika, sababu hii watu hugeuka, feza inatawala popote. Watu wasiotosheka zamani hawahesabu chochote ila feza, kila mmoja hujisumbua kuchuma mali. Popote unawakuta, wanaotafuta mali, penye mashamba ya Wazungu, katika miji mikubwa, watu hawana raha,

ila hulia: 'Feza, feza!' Husema: Wahindi wakikaa pamoja, waongee, wanaongea jinsi wawezavyo kupata feza na faida. Dini inayofaa ni dini ya Wakristo!"

Vijana wanakwenda mbali, watafute kazi, wanauacha ukoo wao, wanasahau kulima mashamba, wanavaa kizungu; vema, lakini wanasahau wazee wao, wasiwaheshimu kwa kipazi. Mama mmoja hashindwi, hulisha hata watoto sita, lakini pengine watoto sita hushindwa kuwalisha baba na mama, kwani wana mengine watakayo. Wazee hujua hali ya watoto wa enzi hii, lakini hawana nguvu ya kuwalea au kuwaonya.

Mashauri ya wazee na ya watoto si mamoja siku hizi. Je, knna nguvu gani, waonywe vema? Sina budi kusema, kama nguvu inatoka katika dini ya kikristo. Zamani vijana wamesikia hata shauri la mjomba na baba, kama wametaka kuoa, leo huchukua wanawake wapendao wao wenyewe, huwatupa wapendavyo, wala hawafuati desturi ya kipazi au desturi ya kizungu au desturi ya kiislamu. Hakuna utaratibu wowote. Wazee wamejua hata shida hii yote, lakini nguvu ya kuwaonya haiko. „Sina nguvu mie, nitende nini"? Hivi husema wazee. Nao vijana hawana raha nao, basi nani atakayeweza kuwasaidia? Ni Bwana Yesu, awezaye kuwaonya kweli kweli na kuwaongoza watu wa enzi hii.

Tamaa zinazidi, huzidi uzinzi, wizi, ugomvi kuliko zamani. Sitaki kuwaambia na kuwaelezea mambo hayo, kwani nyinyi mnajua kuliko mimi. Upazi unapunguka, nguvu yake imekwisha na uzungu hamjaweza bado, basi Ukristo ndio unaowafaa na kuwaponya. Sababu hii inafaa misioni ikiendelea Uzaramo, watu wapate kutunzwa duniani na kupewa mbinguni uzima wa kweli. Wazaramo wakae Wazaramo, lakini wakae Wazaramo wa kikristo, hili ni shauri jema, tena shauri la Bwana Mungu wetu. Ingefaa, Wazaramo wote wakikubali shauri hili.

Mt sion, P. O. Morogoro.

T 52 676 401

Sh. 0,20

Viko **Kalenda** 1929, 1930, 1931, 1932, 1933 na 1934 vinavyo na masimulizi ya nchi nyingi. Sh. 0,20

**Katekisimo** au ufundisho wao Wakristo kama alivyotufundisha D. Martin Luther. Sh. 0,20

**Nyimbo za Kikristo,** tunazomsifu nazo Mungu. Sh. 1,50

**Agano Jipya** la Kiswahili kinachofahamisha vema utume mzuri wa mkombozi Yesu. Sh. 3,—
Katika kifuniko cha ngozi nzuri Sh. 7,50

**Mwongozi wa kufahamu Agano Jipya,** anataka kututambulishia kitabu cha Agano Jipya. Sh. 2,—

**Mwongozi wa kufahamu Agano la Kale,** ameonekana siku hizi vilevile. Sh. 2,75

**Masimulizi na mafundisho.** Kitabu cha kwanza. 1,50

**Hesabuni kwa furaha,** An Arithmetic Method for Teachers of Sub-Standards. Sh. 1,50

**Ufalme wa Mungu** ni Gazeti letu linalotusimulia kila mwezi habari za Mungu, habari za Wakristo wenzetu, habari za ulimwenguni. Kiasi chake ni Ct. 10, mwaka mzima Sh. 1,—

Ukitaka gazeti lako peke yako kila mwezi kwa posta utalipa pamoja na garama ya posta mwaka mzima Sh. 1,60, lakini watu 5 wakipelekewa pamoja na posta, watalipa mwaka mzima Sh. 5,—

## Usambara Agentur

**Misioni Lwandai**


P. O. Lushoto via Tanga, T. T.

a) Garama ya posta inalipiwa na sisi.
b) Kama mtu anaagiza vitabu vingi kwa Shs. 50.—, atapata faida ya Shs. 5.— kwa zile Shs. 50.— (10% discount).
c) Kama bei ni dogo unaweza kulipa na stamp katika barua yako au na Postal Order au na note katika bahasha ya Registered!

---

Imepigwa chapa na Mission Press Vuga, P. O. Mombo, T. T. 3000





# HABARI za WAZARAMO

S 17
12187

Kiasi chake Senti 20.